**TAARIFA KUHUSU MREJESHO WA UHAKIKI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MALIPO KWA MATOKEO AWAMU YA KWANZA NA YA PILI**
**(PAYMENT FOR RESULT- PforR)**

---

## 1. UTANGULIZI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inashirikiana na Washirika wa Maendeleo (*Development Partners*) katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Water Sector Development Programme – WSDP*), ambapo kwa sasa utekelezaji wake upo kwenye Awamu ya Pili iliyoanza mwezi Julai 2016. Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu umejikita katika vipaumbele vilivyoanza kutekelezwa katika Awamu ya Kwanza ikiwa ni pamoja na kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza katika awamu hiyo. Mowapo ya mapungufu hayo ilikuwa ni **uendelevu wa miradi kutokana na mkazo mdogo katika usimamizi wa huduma na matengezo ya miundombinu na hasa kwenye maeneo ya vijijini**. Tathmini iliyofanyika mwishoni mwa Awamu ya Kwanza ya Programu ilionesha pamoja na mambo mengine kuwa vituo vingi vya kuchotea maji viliharibika muda mfupi baada ya kujengwa na kufanya kuwa na zaidi ya asilimia 30 ya vituo vyote kutokutoa maji.

Serikali kupitia Wizara ya Maji inatekeleza Mradi wa *Sustainable Rural Water Supply and Sanitation Program (SRWSP)* ambao unatumia jumla ya **Dola za Kimarekani milioni 350**. Kati ya fedha hizi **Dola za Kimarekani milioni 330** zinatumika kwa ajili ya *Program for Results* (PforR) na kiasi cha **Dola milioni 20** kwa ajili ya *Investment Project Financing (IPF)*, fedha zote zikiwa kwa ajili ya lengo la kukabiliana na kutatua changamoto katika uendelezaji wa Miradi ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Mkataba wa kifedha *(Financial Agreement)* baina ya Serikali na Benki ya Dunia kupitia dirisha lake la IDA ulisainiwa Septemba, 2018.

Programu hii inatekelezwa kwenye mikoa 17 ya Tanzania Bara chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Program hii inakusudia kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini kwa kuzishirikisha Halmashauri za Wilaya 86 zilizopo katika Mikoa 17 kwa kuzijengea uwezo kwa kuchagua mifumo itakayowezesha utoaji wa huduma endelevu.

Mnamo mwezi Septemba, 2019 Benki ya Dunia ilitoa malipo ya awali ya dola milioni 72.5 kwa Serikali ya Tanzania kama mbegu ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa program. Fedha hizi ziligawanywa kwa Wizara ya Afya (USD 11,250,000), Wizara ya Elimu (USD 7,500,000) na Wizara ya Maji (USD 53,750,000). Sehemu ya malipo yaliyopokelewa na Wizara ya Maji, kiasi cha Dola 52,675,000 zilipelekwa kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa kuwa ni watekelezaji wakuu wa miradi ya maji vijijini ambapo dola 51,600,000 zilielekezwa kwa Halmashauri 86 na dola 1,075,000 zilielekezwa katika Ofisi za Mikoa 17.

RUWASA iliwasilisha mipango kazi ya utekelezaji wa shughuli za PforR ambayo imegawanyika katika ujenzi wa miradi mipya ya maji, ukarabati wa miradi ya maji, upanuzi wa miradi ya maji, uimarishaji wa Vyombo vya Watumia Maji (CBWSOs), uboreshaji wa ubora wa maji, na usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za programu. Baada ya kuwasilisha mipango kazi, RUWASA ilipitia na kutoa vibali vya kuendelea na utekelezaji kwa kila Wilaya.

Utekelezaji wa Programu unakwenda kwa mtindo wa motisha, ambapo Halmashauri inayofanya vizuri kwa maana ya kukidhi vigezo (*Disbursed Linked Indicators*) vilivyowekwa ndiyo inayopata fedha nyingi zaidi ikilinganishwa na Halmashauri isiyofanya vizuri kwa vigezo hivyo hivyo. Kiwango cha malipo ya motisha au bonasi kinategemeana na jinsi Halmashauri inavyokidhi hivyo vigezo baada ya uhakiki na tathmini inayofanywa na Timu ya Wataalam wa Kujitegemea (Independent Verification Agent) – IVA). Kwa sasa uhakiki wa Programu huu unafanywa na

Kampuni ya PEM Consult chini ya Usimamizi wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani (IAG) ambao ndiyo wenye dhamana hiyo.

Kwa Upande wa RUWASA kuna vigezo vikuu vinne (4) vinavyozingatiwa katika kupata bonusi au motisha. Vigezo hivyo, ni kama ifuatavyo: -

(i) Uwepo wa ongezeko la idadi ya watu wapya wanaopata huduma ya Maji (DLI 1);
(ii) Uwepo wa uendelevu wa vituo vinavyofanya kazi (DLI 2)
(iii) Uwepo wa vijiji vinavyohudumiwa na Chombo cha Watumiaji Maji (DLI 6)
(iv) Uwasilishaji, usahihi wa takwimu na taarifa za huduma ya maji kila mwezi (DLI 7
(v) Uanzishwaji wa Taasisi ya RUWASA (*RUWASA establishment (DLI 8*).

Vigezo na masharti yote ya Programu hii vinauwiana na viwango vya kitaifa vya kisekta katika utoaji wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira. Taarifa au takwimu zinazotumika katika tathmini ni taarifa rasmi za kila mwezi zinazokusanywa na timu maalum ya kukusanya, kutunza na kusambaza takwimu za maji vijijini (CDMT). Tathmini hufanywa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza inahusu uhakiki wa ndani ya RUWASA ili kujiridhisha na **ukamilifu**, **ukweli** na **ubora wa taarifa** zilizokusanywa. Awamu ya pili ni uhakiki wa nje unaofanywa na timu huru niliyoitaja inayosimamiwa na Washirika wa Maendeleo.

Makubaliano yaliyopo kati ya Wizara ya Maji na wadau ni kuwa, kila mwaka Timu hiyo huru itafanya uhakiki wa vituo vya kuchotea maji vijijini. Matokeo ya uhakiki huo ndiyo yanayotumika katika kuamua Halmashauri zilizokidhi vigezo na kukokotoa malipo ya motisha au bonasi stahili kwa kila Halmashauri. Utaratibu wa kupata malipo ya motisha kwa kila Halmashauri ni kama ifuatavyo: -

(i) Halmashauri itapata **USD 25** (sawa na takriban **Sh.57,000**) kwa kila ongezeko la idadi ya watu wapya waopata huduma ya maji

(ii) Halmashauri itapata **USD 164** (sawa na takriban **Sh. 375,000**) kwa uwepo wa uendelevu wa kituo cha kuchotea maji

(iii) Halmashauri itapata **USD 15,000 (sawa na takribani Sh. 68,000** kwa kila kijiji ambacho kinahudumiwa na Chombo cha Watumiaji Maji (CBWSO)

(iv) Halmashauri itapata kiasi cha jumla (*lumpsum amount*) itakayolipwa kwa kuzingatia usahihi (***accuracy level)*** wa taarifa na takwimu zinazowasilishwa kila mwezi. Kiasi hicho ni **USD 23,000** (sawa na takriban **Sh. 52,000,000**)

Mbali ya bonasi inayokokotolewa kwa vigezo nilivyoeleza, ambayo huelekezwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa mipango ya kuboresha huduma ya maji vijijini katika Halmashauri husika, kuna fedha zinazoelekezwa kwenye Ofisi za Mikoa na Makao Makuu ya RUWASA kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu. Kwa upande wa mikoa, kila mkoa unapata **asilimia 2** ya jumla ya fedha inayolipwa kwa Halmashauri zote zilizo ndani ya mkoa huo. Halikadhalika, kwa upande wa RUWASA Makao Makuu, fedha inayolipwa ni **asilimia 2** ya fedha zote zitakazolipwa kwa Halmashauri na Mikoa.

Mfumo huu wa utoaji wa fedha za utekelezaji wa Programu unalenga kuhamasisha na kuchochea utamaduni wa **kutunza**, **kuendeleza** na **kukarabati miundombinu ya maji** ili kuhakikisha kuwa huduma ya maji vijijini inakuwa endelevu. **Fedha hizi hazitumiki katika shughuli za**

**kiutumishi na kiutawala kama vile kulipa mishahara na kulipa ankara za umeme na mafuta ya kuendeshea mitambo ya kusukuma maji**.

Fedha hizi zimekua zikitumika katika maeneo yafuatayo,

(i) Kuongeza upatikanaji wa huduma za maji kwa kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya maji katika maeneo ya vijiji na miji midogo na makao makuu ya Wilaya;

(ii) Kuimarisha uendelevu wa upatikanaji wa huduma za maji kwa kuongeza vituo vya kuchotea maji na maunganisho ya majumbani.

(iii) Kuongeza ubora wa maji na huduma za maji ikiwa ni pamoja usajili wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSO Level I & II)

(iv) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

## 2. UHAKIKI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA PforR 2019/2020 AWAMU YA 1 & AWAMU YA 2

Katika Awamu hii ya kwanza (2019/2020), Halmashauri zilizofuzu baada ya uhakiki na tathmini ni 86 ambapo jumla ya **Shilingi Bilioni 186** zimetolewa, ikiwa ni ongezeko la takriban Shilingi Bilioni 67 kulinganisha na kiasi kilichotolewa kama mbegu. Hata hivyo, pamoja na ongezeko hilo la fedha, bado kuna maeneo kadhaa ambayo tathmini imeonesha kuwa baadhi ya Halmashauri hazikufanya vizuri katika vigezo nilivyovitaja.

Awamu ya Pili ya Uhakiki wa Programu ya Malipo kwa Matokeo (PforR) uliofanyka katika Mikoa 17 ukihusisha Halmashauri 86 umewezesha Halmashauri kupata jumla ya Dolla za Kimarekani USD 11,286,098 sawa na **Shilingi Bilioni 250,393,720,500.** Ambayo ni sawa na ongezelo la asilimia 34 toka malipo/mavuno ya awamu ya kwanza. Hata hivyo, pamoja na jitihada zilizofanyika hadi upatikanaji wa kiasi hicho cha fedha, zoezi la uhakiki lilikumbwa na changamoto ya mlipuko wa ugonjwa wa Covid 19 (Corona Virus) hali iliyopelekea baadhi ya maeneo kushindwa kupata taarifa sahihi kwa wakati.

## 3. WASHINDI KATIKA UTEKELEZAJI WA PRORAMU YA PforR

Katika kutambua utendaji kazi mzuri wa watekelezaji wa Programu hii katika ngazi ya Wilaya na Mkoa, RUWASA Makao Makuu imeona kuwa ipo haja ya kutambua Ofisi za RUWASA za Wilaya na Mikoa zilizowezesha Halmashauri kufanya **vizuri** na kwa ridhaa yako tutaomba uwatunuku vyeti maalum katika hafla hii. Tumeandaa makundi matano ya vigezo katika kupata Halmashauri 3 zilizofanya vizuri kwa kila kigezo. Vigezo hivyo ni kama ifuatavyo: -

(i) Utendaji DLI-1: Ongezeko la watu wapya wanaopata huduma ya maji (New population increase) ngazi ya Halmashauri.

(ii) Utendaji DLI-2: Uendelevu wa vituo vya kuchotea maji na maunganisho ya majumbani ngazi ya Halmsahuri

(iii) Utendaji DLI-6 Ongezeko la usajili wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji ngazi ya Jamii ngazi ya kwanza na pili (CBWSO Level I & II) Ngazi ya Halmashauri

(iv) Utendaji wa Jumla Ngazi ya Halmashauri

(v) Vigezo vya jumla vya kiutendaji (*overall performance*) katika ngazi ya Mkoa.

Halmashauri zilizofanya vizuri na vibaya sana katika kila kigezo ni kama ifuatavyo: -

**(i) Utendaji DLI-1: Ongezeko la watu wapya wanaopata huduma ya maji (New population increase) ngazi ya Halmashauri**

Uchambuzi wa matokeo kupitia Program ya Malipo kwa Matokeo (PforR) umebainisha kuwa, Halmashauri za Kakonko, Mbulu na Uyui zimeongoza kwa kufanya vizuri katika kigezo cha utendaji DLI-1 kwa kuongeza idadi ya watu wapya wanaopata huduma ya maji kati ya Halmashauri 86 zilizopo katika Programu hii. Matokeo ya DLI-1 yamechambuliwa kama ifuatavyo,

**a)** DLI 1: Halmashauri zilizofanya vizuri

| Na. | HALMASHAURI | Ongezeko la watu wapya wanaopata huduma ya maji (AWAMU YA 1) | Ongezeko la watu wapya wanaopata huduma ya maji (AWAMU YA 2) |
|---|---|---|---|
| 1. | Kakonko | 0 | 68,571 |
| 2. | Mbulu | 22,413 | 63,239 |
| 3. | Uyui | 45,680 | 58,199 |

Uchambuzi wa matokeo kupitia Programu ya Malipo kwa Matokeo (PforR) umebainisha kuwa, Halmashauri za Kakonko, Mbulu na Uyui zimeongoza kwa kufanya vizuri katika kigezo cha utendaji DLI-1 kwa kuongeza idadi ya watu wapya wanaopata huduma ya maji.

b**) DLI 1: Katika Awamu ya Pili, Halmashauri ambazo hazikufanya vizuri** ni pamoja na Biharamulo, Busega, Igunga, Ikungi, Itilima, Kilolo, Kilwa, Kishapu, Kiteto, Madaba, Magu, Maswa, Mbogwe, Mkalama, Momba, Mpimbwe, Muleba, Nyasa, Rorya, Sikonge, Singida, Tandahimba, Urambo na Uvinza.

**(ii) Utendaji DLI-2: Uendelevu wa vituo vya kuchotea maji na maunganisho ya majumbani ngazi ya Halmsahuri**

Uchambuzi unaonesha kuwa, Halmashauri za **Mbogwe, Buhigwe, Masasi**, zimeongoza kwa kufanya vizuri katika kuhakikisha uendelevu wa vituo vya kuchotea maji na maunganisho ya majumbani kupitia DLI-2. Kufuatia uendelevu huo, Halmashauri ya Mbogwe imeongoza kwa kuwa na wastani mkubwa wa asilimia 97.89 kwa vituo vya kijamii vya kuchotea maji na maunganisho ya majumbani. Aidha, Halmashauri 3 kama zinavyoonekana kwenye jedwali hapa chini zimeonesha kutopata matokeo kabisa kwa kukosa kuwa na ongezeko la vituo vya kijamii vya kuchotea maji (WP) na maunganisho ya majumbani (HHC) hivyo kupelekea wananchi kukosa uwezeshaji wa kutosha kupata huduma ya maji kupitia Program hii. Uchambuzi wa matokeo ya DLI-2 ni kama ifuatavyo: -

a) **DLI 2: Halmashauri zilizofanya vizuri**

| Na. | HALMASHAURI | Wastani wa uendelevu wa vituo vya kuchotea maji (%) (AWAMU YA 1) | Wastani wa uendelevu wa vituo vya kuchotea maji (%) (AWAMU YA 2) |
|---|---|---|---|
| 1. | MBOGWE | 69 | 96 |
| 2. | BUHIGWE | 95 | 95 |
| 3. | MASASI | 81 | 94 |

b) **DLI-2: Halmashauri zilizofanya vibaya**

Katika Awamu ya Pili, Halmashauri ambazo hazikufanya vizuri ni pamoja na **Musoma, Mkalama, Mbozi, Mlele, Nsimbo, Lindi, Kiteto, Simanjiro, Rorya, Serengeti, Newala, Mbinga, Itilima, Maswa na Igunga**

**(iii) Utendaji DLI-6 Ongezeko la usajili wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji ngazi ya Jamii ngazi ya kwanza na ya pili (CBWSO Level I & II) Ngazi ya Halmashauri**

Uhakiki umeonesha kuwa, Halmashauri za **Nzega, Masasi na Igunga** zimepata matokeo mazuri kwa kuongeza usajili wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii kutoka ngazi ya kwanza kwenda ngazi ya pili (CBWSO Level I & II). DLI-6 (CBWSO Level I & II):

a) **Halmashauri zilizofanya vizuri**

| Na. | HALMASHAURI | IDADI YA VIJIJI VINAVYOHUDUMIWA NA CBWSO (AWAMU YA 1) | JUMLA YA MATOKEO (AWAMU YA 1) | IDADI YA VIJIJI VINAVYOHUDUMIWA NA CBWSO (AWAMU YA 2) | JUMLA YA MATOKEO (AWAMU YA 2) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Nzega | 17 | 1,113,750,000 | 115 | 7,762,500,000 |
| 2. | Masasi | 34 | 1,147,500,000 | 84 | 4,623,750,000 |
| 3. | Igunga | 14 | 911,250,000 | 70 | 4,623,750,000 |

b) **Halmashauri zilizofanya vibaya**

| Na. | HALMASHAURI | IDADI YA VIJIJI VINAVYOHUDUMIWA NA CBWSO (AWAMU YA 1) | JUMLA YA MATOKEO (AWAMU YA 1) | IDADI YA VIJIJI VINAVYOHUDUMIWA NA CBWSO (AWAMU YA 2) | JUMLA YA MATOKEO (AWAMU YA 2) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Itigi | 2 | 67,500,000 | 4 | 270,000,000 |
| 2. | Ushetu | 7 | 472,500,000 | 3 | 202,500,000 |
| 3. | Mbogwe | 12 | 810,000,000 | 2 | 135,000,000 |

**(iv) Utendaji wa Jumla Ngazi ya Halmashauri**

**a)** Matokeo ya jumla yanaonesha kuwa, Halmashauri za Nzega, Masasi, Uyui, zimeshika nafasi Tatu bora kati ya Halmashauri 86 katika kigezo cha utendaji wa jumla ngazi ya Halmashauri. Kigezo cha ujumla cha kiutendaji Halmashauri zilizofanya vizuri.

| **Na.** | **HALMASHAURI** | **KIASI (Tsh.)** |
|---|---|---|
| 1. | Nzega | 10,219,270,500 |
| 2. | Masasi | 6,615,585,000 |
| 3. | Uyui | 6,581,535,750 |

**a) Kigezo cha ujumla cha kiutendaji Halmashauri zilizofanya vibaya**

| **Na.** | **HALMASHAURI** | **KIASI (Tsh.)** |
|---|---|---|
| 1. | Mbogwe | 354,051,000 |
| 2. | Uvinza | 413,181,000 |
| 3. | Madaba | 500,130,000 |

**(v) Utendaji wa Jumla Ngazi ya Mkoa**

Uhakiki umebaini kuwa, Mikoa ya Tabora, Kagera, Mara imeshika nafasi tatu za juu kupitia kigezo cha ujumla cha utendaji ngazi ya Mikoa kwa kufanya vizuri kati ya Mikoa 17 inayotekeleza miradi ya maji kupitia Programu ya Malipo kwa Matokeo. Uwezeshaji huu utasaidia kukamilisha miradi ya maji inayotekelezwa katika maeneo hayo na hatimae kuleta tija kwa wananchi kupata huduma ya maji kwa wakati. Kigezo cha ujumla cha kiutendaji Mikoa iliyofanya vizuri.

| **Na.** | **MIKOA** | **BONASI (Sh.)** | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **Kiwango cha fedha Awamu ya 2** | **Wastani kwa Halmashauri Awamu ya 2** | **Wastani kwa Halmashauri Awamu ya 1** |
| 1. | Tabora | 26,678,540,250 | 4,446,423,375 | 3,234,457,425 |
| 2. | Rukwa | 11,646,553,500 | 3,882,184,500 | 1,257,906,900 |
| 3. | Iringa | 10,963,896,750 | 3,654,632,250 | 1,874,792,400 |

a) **Mikoa ambayo haikufanya vizuri**

| Na. | MIKOA | BONASI (Sh.) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **Kiwango cha fedha Awamu ya 2** | **Wastani kwa Halmashauri Awamu ya 2** | **Wastani kwa Halmashauri Awamu ya 1** |
| 1. | Geita | 8,293,259,250 | 1,658,651,850 | 2,205,852,120 |
| 2. | Shinyanga | 6,959,369,250 | 1,739,842,313 | 2,110,951,913 |
| 3. | Katavi | 7,468,501,500 | 1,867,125,375 | 3,574,257,750 |

## 4. HITIMISHO

Mafanikio katika utekelezaji wa Mpango huu yanatengemea sana utendaji kazi na ushirikiano wa karibu wa watekelezaji na wasimamizi yaani Jumuiya za Watumia Maji, Wahandisi wa Maji na Mafundi Sanifu, Mameneja wa Wilaya na Mikoa na RUWASA Makao Makuu. Jambo muhimu ni kuwa na uelewa wa vigezo vya Mpango huu na kusimamia kikamilifu utekelezaji wake.

Kwa kutambua hilo, tuliona kuwa ipo haja ya kuwakutanisha watendaji wakuu wa Programu yaani Mameneja wa RUWASA wa Mikoa na Wilaya ili wapate fursa ya kupata mrejesho wa uhakiki na tathmini ya utekelezaji wa Programu katika Awamu ya Nne utakaowasilishwa na Wataalam waliofanya kazi hiyo. Ni matumaini yangu kuwa fursa hii itakuwa ni chachu ya kuboresha utendaji kazi wao ili kuongeza bonasi na hatimaye kuongeza kasi ya kuwapatia wananchi waishio vijijini huduma ya uhakika ya maji safi na salama.

Eng. Clement KIVEGALO
**MKURUGENZI MKUU – RUWASA**
23 Februari, 2022